SHULE YA UPILI YA WAMY

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA

KAZI YA LIKIZO 2020

KISWAHILI-KARATASI MSETO

KIDATO CHA TATU

JINA: _____ DARASA: _____

TAREHE: _____ SAHIHI: _____ NAMBARI YA MTAHINIWA: _____

Maagizo

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

(c) Jibu maswali ***yote.***

(d) Majibu yako yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

(e) Majibu yote ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya* ***Kiswahili****.*

(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

(g) Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.

(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1.Ufahamu	10	
2. Matumizi ya Lugha	30	
3. Isimujamii	10	
4. Fasihi Simulizi	10	
5. Fasihi Andishi	20	
Jumla	80	

@ 2020Wamy High School

Geuza ukurasa

1. UFAHAMU : ALAMA10

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo:

Nimekaa kutafakari kwa kipindi kirefu juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake.Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao.Kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho.Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengikatika unyanyasaji,kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kutkana na mafanikio haya,wabunge waliopitisha hoja bungeni za kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa.Mafanikio haya yamewafanya kina mama kujikimu kimaisha,na hivyo kutowategemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili,nenda kwenye masoko utaona akina mama jinnsi wanavyohangaika na biashara zao.Kwa hivyo,ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali na fedha.Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maish ya heshima.Wale ambao hawajaribu kuchukua mkopo ni muhimu wafanye hivyo iliwajikimu kimaisha.Maisha ya sasa ni magumu,hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali.Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki.Ushirikiano utarahisisha maisha yao,hata hivyo,sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao,toka kwa akina baba,bali hata masualama ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama,zimepungua.Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika kinyume na hapo awali,amabapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikua hifadhi ya wanaume,siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

MASWALI:

(a) Taja dhamira moja ya makala haya. (Alama 1)

_____

(b) Eleza ni kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge. (Alama1)

_____

_____

(c) Wanaume walikuwa wakirudisha nyuma maendeleo nchini kivipi? (Alama 2)

_____

_____

(d) Sera za serikali zimesaidia wanawake kivipi? (Alama 2)

_____

_____

(e) Eleza ni kwa nini baadhi ya wanawake wanaishi katika lindi la umaskini. (Alama 2)

_____

_____

(f) Eleza maana ya msamiati na mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika makala haya:

(i) Kutafakari_____ (Alama 1)

(ii) Kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji (Alama 1)

_____

2. MATUMIZI YA LUGHA : ALAMA 30

(a) Ainisha mofimu za neno hili:
Kitanda (Alama 2)

_____

_____

(b) Onyesha jinsi neno 'kwetu' lilivyotumika katika sentensi zifuatazo: (Alama 2)

(i) Kwetu ni huku._____

(ii) Mahali kwetu ni huku._____

(c) Kwa kutunga sentensi,onyesha shamirisho kipozi,shamirisho kitondo na shamirisho ala.(Alama 3)

_____

_____

(d) Andika kwa usemi wa taarifa: (Alama 3)
"Njoo hapa!Babu aliwaamuru.

_____

(e) Geuza sentensi hii hadi udogo. (Alama 2)
Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi.

_____

(f) Tunga sentensi moja yenye kirai kivumishi na kirai kielezi. (Alama 2)

_____

(g) Yakinisha sentensi hii: (Alama 2)
Mjomba hakulima shamba wala kuenda safarini.

_____

(h) Andika kinyume cha sentensi hii. (Alama 3)
Mvulana aliingia kwenye nyumba na kutawanya maembe.

_____

(i) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi: Umba (Alama 2)

_____

_____

(j) Tambua na ueleze vitenzi vilivyotumika katika sentensi ifuatayo: (Alama 3)
Shipiri ni mzuri inagawa huenda akaharibiwa na Halima ambaye si msichana mwema.

_____

_____

_____

(k) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (Alama 6)
Waliompiga vibaya sana wametorokea msituni.

_____

_____

_____

_____

_____

3. ISIMUJAMII : ALAMA 10

"Kutokana na kufungwa kwa maabara,kikundi chetu hakitamaliza utafiti ulioratibiwa kukamilishwa mwishoni mwa mwezi ujao."

(a) Tambua sajili ya mazungumzo haya. (Alama2)

_____

(b) Fafanua sifa nne za sajili uliotaja katika swali la (i). (Alama 8)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

4 . FASIHI SIMULIZI: ALAMA 10

(a) Maghani ni nini? (Alama 2)

_____

_____

(b) Eleza aina zifuatazo za maghani: (Alama 8)

(i) Tondozi

_____

_____

(ii) Sifo

_____

_____

(iii) Tendi

_____

_____

(iv) Rara

_____

_____

5. FASIHI ANDISHI

Kigogo-Pauline Kea : ALAMA 10

(a) "Mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake Ashua.Tamaa ilimuua fisi."

(i) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (Alama 2)

(ii) Bainisha tamathali za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (Alama 2)

(iii) Fafanua sifa mbili za msemewa. (Alama 2)

(iv) Ukirejelea tamthilia nzima fafanua maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (Alama 4)

Geuza ukurasa

(b) **USHAIRI** : **ALAMA 10**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:

Msituni nikakuta,nyuki wamo mzingani,
Kwa juhudi wanakita,mara nje mara ndani,
Husuda wameikata,hata hawasengenyani,
Nyuki ni wadudu duni,wanashinda kwa umoja,

Mchwa nao nikaona,wamejenga masikani,
Wafanya bidii sana,uvivu hawatamani,
Wao husaidiana tena,hawadanganyani,
Mchwa wadudu wa chini,wanaishi kwa umoja,

Nalo jeshi la siafu,hutandawaa njiani,
Laenda bila hofu,maana lajiamini,
Silaha zao dhaifu,meno,tena hawaoni,
Wa kuwatadia nini?kwani wanao umoja.

Nao chungu wachukuzi,nyama warima njiani,
Maskini wapagazi,mizigo yao kichwani,
Ingawa si wachokozi,wakali ukiwahini,
Katu hawafarakani,wanadamu kwa umoja.

Sisi ni wana Adamu,mbona hatusikizani
Tusitietie hamu,ukubwa kuutamani,
Wachache wataalamu,tuwasadi kwa imani,
Hii"Huyu awezani,"yatuvunjia umoja.

Maswali:

(i) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama1)

_____

(ii) Eleza muundo wa shairi hili. (Alama 2)

_____

_____

_____

_____

(iii) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (Alama 2)

_____

_____

_____

_____

(iv) Taja na uthibitishe mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika shairi. (Alama 1)

_____

_____

(v) Shairi hili ni la bahari gani? Eleza. (Alama 2)

_____

_____

(vi) Onyesha jinsi mtunzi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili. (Alama 2)

_____

_____

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

@ 2020 Wamy High School